PENTECOSTAL ASSEMBLIES OF GOD TANZANIA

HEAD OFFICE: P. O. BOX 3390 DODOMA, TANZANIA. Tel. 026-2350019

# PENTECOSTAL ASSEMBLIES OF GOD TANZANIA

# KATIBA YA KANISA LA PAG (T)

# YA MWAKA 2017

# NA

# KANUNI CHINI YA IBARA YA 44

## DIBAJI

*Kanisa la Pentecostal Assemblies of God (Tanzania)ni Kanisa la Kipentekoste lenye msingi na imani katika Neno la Mungu. Kanisa hili linaundwa na ujumla wa makanisa ya mahali pamoja. Lilianzishwa chini ya wamisionari waliotoka Kanada wakiwa chini ya Shirika la kimisionari liitwalo Pentecostal Assemblies of Canada.Wa misionari hao walianza kueneza Injili Tanganyika katika mazingira magumu tangu miaka ya 1912. Katika miaka hiyo wengine walifariki kwa magonjwa na kuzikwa hapa nchini bila juhudi zao kubwa kuonekana kama zinazaa matunda wakati huo. Baada ya wamisionari wa kwanza kufariki* waliofuata walikuja *wamejipanga zaidi na kuanzis ha shule ya Biblia kule Nyang'ori Kenya kwenye miaka ya 1950 ambako wahubiri wa mwanzo wa Tanganyika walipewa mafunzo. Baada ya watumishi hao kurudi*

*Tanganyika Kanisa hili lilianza katika mkoa wa Mara na kuanzisha shule ya Biblia pale Nyasirori Butiama. Wakati huo lengo kuu lilikuwa kuhubiri Injili na kuanzisha makanisa. Kwa kuwa Kanisa lilizidi kuongezeka na mambo ya utawala kuwa muhimu ilibidi Kanisa hili liandikishwe rasmi na liwe na uongozi wake, Kanisa liliandikishwa tarehe 14 Aprili mwaka 1967 na kupata "Certificate of Incorparation" baada ya kuwa na makanisa*

*katika mikoa ya Kanda ya Ziwa. Kwa kuwa Katiba ya mwanzo, iliyotumika kuliandikisha Kanisa hili, haikukidhi tena kiwango cha ukuaji wa Kanisa na matakwa ya kisheria, ilifanyiwa marekebisho tena mwaka wa 1985 na kutumika kuliandikisha Kanisa chini ya Msajili wa vyama tarehe 23 Octoba 1987, Hati ya Usajili NA. SO. 6510.*

*Kwa hiyo Katiba hii ya mwaka 2017 ni marekebisho ya Katiba ya Muda ya* ***PAG (T)*** *ya mwaka 1985 ambayo imezingatia mabadiliko yaliyotokea katika* ***PAG (T)*** *kwa kipindi chote kilichopita. Kanisa hili limeweza kuenea toka Kanda ya Ziwa mpaka sehemu yingine zaTanzania.Maba diliko haya yalilazimu hata makao makuu ya Kanisa la* ***PAG (T)*** *kuhama kutoka Mwanza kwenda Dodoma. Kwa kuwa mchakato mzima wa kupata Katiba hii umeshirikish a wadau wengi toka ngazi za chini hadi juu, hivyo Katiba hii inatazamiwa kulisaidia Kanisa kueneza injili katika mazingira yenye amani, utulivu, na mshikamano wa washirika wa Kanisa la* ***PAG (T)*** *na wadau wake.*

# YALIYOMO

**DIBAJI ... ii**

**YALIYOMO ... iv**

**SURA YA 1: UTAMBULISHO WA KANISA NA USHIRIKA ... 1**

IBARA YA 1: JINA LA KANISA ... 1

IBARA YA 2: NEMBO YA KANISA LA PAG (T) ... 1

IBARA YA 3: ENEO LA KAZI NA MAKAO MAKUU YA KANISA ... 1

IBARA YA 4: DIRA NA DHAMIRA YA KANISA LA PAG (T) ... 2

IBARA YA 5: SHABAHA ZA KANISA LA PAG (T) ... 2

IBARA YA 6: TAMKO LA IMANI YA KANISA LA PAG (T). ... 3

IBARA YA 7: TUNU ZA KANISA ... 6

IBARA YA 8: MAAGIZO MAKUU ... 6

IBARA YA 9: USHIRIKA ... 7

**SURA YA 2: USIMAMIZI WA MALI ZA KANISA ... 11**

IBARA YA 10: WADHAMINI WA KANISA ... 11

**SURA YA 3: MIKUTANO, MABARAZA NA KAMATI ... 17**

IBARA YA 11: MKUTANO MKUU ... 17

IBARA YA 12: HALMASHAURI KUU ... 18

IBARA YA 13: BARAZA LA WAANGALIZI ... 22

IBARA YA 14: JIMBO ... 23

IBARA YA 15: WILAYA ... 27

IBARA YA 16: KAMATI YA ASSEMBLI ... 31

IBARA YA 17: KANISA LA MAHALI ... 32

**SURA YA 4: VIONGOZI WA KANISA LA PAG (T) ... 36**

IBARA YA 18: ASKOFU MKUU ... 36

IBARA YA 19: MAKAMU ASKOFU MKUU ... 39

IBARA YA 20: KATIBU MKUU ... 40

IBARA YA 21: NAIBU KATIBU MKUU ... 42

IBARA YA 22: ASKOFU WA JIMBO ... 43

IBARA YA 23: MAKAMU ASKOFU WA JIMBO ... 45

IBARA YA 24: KATIBU WA JIMBO ... 46

IBARA YA 25: NAIBU KATIBU WA JIMBO ... 48

IBARA YA 26: MWANGALIZI WA WILAYA ... 49

IBARA YA 27: MAKAMU MWANGALIZI WA WILAYA ........................................ 50
IBARA YA 28: KATIBU WA WILAYA. ........................................ 51
IBARA YA 29: NAIBU KATIBU WA WILAYA. ........................................ 53
IBARA YA 30: MWANGALIZI WA ASSEMBLI ........................................ 54
IBARA YA 31: KATIBU WA ASSEMBLI ........................................ 55
IBARA YA 32: MCHUNGAJI WA KANISA LA MAHALI ........................................ 55
IBARA YA 33: KATIBU WA KANISA ........................................ 58
**SURA YA 5: MAMBO MBALIMBALI YA KANISA ........................................ 59**
IBARA YA 34: KUPIGA KURA ........................................ 59
IBARA YA 35: IDARA ZA PAG (T) ........................................ 60
IBARA YA 36: HUDUMA ZA JAMII ........................................ 61
IBARA YA 37: KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA KIOFISI. ........................................ 61
IBARA YA 38: UHUSIANO WA PAG (T) NA MASHIRIKA MENGINE ........................................ 63
IBARA YA 39: MAWASILIANO ........................................ 63
IBARA YA 40: UTARATIBU WA KUTATUA MIGOGORO ........................................ 64
IBARA YA 41: UTUMISHI ........................................ 64
IBARA YA 42: NDOA ........................................ 65
IBARA YA 43: MAPATO NA MATUMIZI YA PESA ........................................ 65
IBARA YA 44: SHERIA NDOGO NDOGO ........................................ 66
IBARA YA 45: MAREKEBISHO YA KATIBA ........................................ 66
**KATIBA YA PAG (T) YA MWAKA 2017. ........................................ 67**
**KANUNI CHINI YA IBARA YA 44. ........................................ 67**
**UTANGULIZI ........................................ 67**
**SEHEMU YA KWANZA: UFAFANUZI WA IBARA ZA KATIBA. ........................................ 67**
Sura ya 2 - Ibara ya 10 B (1). ........................................ 67
Sura ya 2 - Ibara ya 10 E (1) na G (8). ........................................ 67
Sura ya 3 - Ibara ya 11 (F). ........................................ 68
Sura ya 3- Ibara ya 11 (i). ........................................ 68
Sura ya 3 - Ibara ya 14 A (4), B (4). ........................................ 68
Sura ya 3- Ibara ya 15 (B) 2. ........................................ 68
Sura ya 3 - Ibara ya 15 (B) 7. ........................................ 68
Sura ya 3 -Ibara ya 17 (c) (3,4). ........................................ 69
Sura ya 4 - Ibara ya 32 a (7). ........................................ 70

SIFA ZA KUSIMIKWA KWA MCHUNGAJI.......70
Sura ya 4 - Ibara ya 32 B.......70
Sura ya 5 -Ibara ya 34 (B).......71
Sura ya 5- Ibara ya 35 (B).......72
Sura ya 5- Ibara ya 36 (A-B).......72
Sura ya 2 - Ibara ya 10 (C), 3,4; na Sura ya 2 Ibara ya 37 (A-K).......72
Sura ya 5- Ibara ya 38 ya (A-C).......72
Sura ya 5- Ibara ya 39 (A).......73
Sura ya 5- Ibara ya 41 (B). HAKI ZA WATUMISHI.......73
Sura ya 5 -Ibara ya 42.......74
Sura ya 5 - Ibara ya 43 (a) (b).......75
Sura ya 5- Ibara ya 44.......77
Sura ya 5 - Ibara ya 45.......77
**SEHEMU YA PILI: MENGINEYO.......77**

## SURA YA 1: UTAMBULISHO WA KANISA NA USHIRIKA

### IBARA YA 1: JINA LA KANISA

Kanisa hili litaitwa **Pentecostal Assemblies of God (Tanzania).**Kwa kifupi **PAG (T).**

### IBARA YA 2: NEMBO YA KANISA LA PAG (T)

Nembo ya Kanisa la **PAG (T)** itakuwa na mambo yafuatayo:

**A.** Ramani ya Dunia ni kuelezea kuwa tunatimiza Agizo Kuu la Bwana Wetu Yesu Kristo (Mat. 28:19-20).

**B.** Alama ya Msalaba inaonesha kuwa tunaikubali kazi ya Yesu pale Msalabani (1 Kor. 1:18).

**C.** Biblia inaonesha Neno la Mungu (2 Tim. 3:16).

**D.** Alama ya Njiwa/Hua inaonesha kuwa tunaami-ni Ubatizo wa Roho Mtakatifu na kazi zake kwa Kanisa na ulimwengu (Mat. 3:16).

### IBARA YA 3: ENEO LA KAZI NA MAKAO MAKUU YA KANISA

**A.** Kanisa la Pentecostal Assemblies of God (Tanzania) litafanya kazi katika eneo lote la

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nje ya nchi.

**B.** Makao makuu yake yatakuwa Dodoma.

**IBARA YA 4: DIRA NA DHAMIRA YA KANISA LA PAG (T)**

**A.** Dira ya Kanisa la **PAG (T)** ni kuwa Kanisa linalombadilisha kila mtu kwa Injili ya Kristo kiroho, kimwili na katika nafsi yake.

**B.** Dhamira ya **PAG (T)** ni kumwabudu Mungu katika roho na kweli na kuihubiri Injili katika nguvu za Roho Mtakatifu kwa kila mtu na kila mahali, kuanzisha na kuimarisha makanisa ya mahali yatakayokuwa chumvi na chachu ya mabadiliko kuleta ufalme wa Mungu kwa watu wake na viumbe vyote.

**IBARA YA 5: SHABAHA ZA KANISA LA PAG (T)**

**A.** Kuhubiri Injili kwa kila kiumbe na kufundisha Neno la Mungu ili kuwafanya walioamini kuwa wanafunzi wa Yesu.

**B.** Kuanzisha na kuimarisha makanisa mijini, vijijini na kila mahali wanakoishi watu;makanisa yanayomtii Kristo na kuieneza Injili yake; na

makanisa yenye uwezo wa kujieneza, kujitegemea na kuihudumia jamii mahali yaliko.

**C.** Kuweka tayari mafundisho mema ya kikristo kwa washirika wote kwa njia ya vitabu, mafundisho ya shule za Biblia, mikutano ya Injili na semina,mafundisho kwenye radio, runinga ya takayowaimarisha washirika kiroho, kiakili, na kimwili.

**D.** Kuanzisha taasisi za elimu ili kutimiza malengo na dira ya Kanisa.

**E.** Kuendesha miradi na huduma za jamii.

## IBARA YA 6: TAMKO LA IMANI YA KANISA LA PAG (T).

**TUNAAMINI**:

**A.** Kwamba kuna Mungu mmoja mwenye enzi ya milele katika Utatu: Mungu Baba,Mungu Mwana,na Mungu Roho Mtakatifu. (Kumb. 6:4; Mk. 12:29; Mt 28:19; 2 Kor. 13:14).

**B.** Katika uumbaji mkamilifu wa Mungu kwa binadamu, mume na mke, kwa mfano wake, na viumbe vyote, na kwamba kulikuwa na anguko la malaika na mwanadamu ambalo matokeo yake yameleta maumivu na uharibifu na kifo

cha kiroho na cha kimwili.
(Mwa.1:1,26-27,31;3:1-19; Rum.3:23).

**C.** Biblia imevuviwa na Mungu,ni Neno la Mungu lenye mamlaka na lisilokuwa na makosa nayo ndiyo msingi wa imani yetu na mwenendo wa kikristo (2 Tim 3:15-17;2 Pet.1:21).

**D.** Katika Uungu wa Bwana wetu Yesu Kristo,katika kuzaliwa kwake na bikira huyo ni Mariamu,katika maisha yake yasiyo na dhambi,katika miujiza yake,katika kifo chake badala ya wenye dhambi ambacho kilifanyika upatanisho kati ya mwanadamu na Mungu, na katika ufufuo wake katika mwili na kupaa kwake mbinguni na kukaa mkono wa kuume wa Mungu Baba,na katika kurudi kwake mara ya pili hapa duniani katika nguvu na utukufu ili kuyatawala Mataifa. (Mt.1:18-23;16:15-16;Mk.16:19;Mdo.1:9-11;2 Kor.5:17;Kol.1:15).

**E.** Kwamba njia pekee ya wokovu wa binadamu kutoka dhambini ni kutubu na kuacha dhambi na kumwamini Bwana Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yake na kwa kuzaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu.(Yoh.1:11-13;3:5-8;Mdo.2:38;Rum.10:9;1Yoh.1:9)

**F.** Katika kuponywa kwa mwili wa binadamu ambako kumepatikana kwa njia ya kifo cha Yesu Kristo pale msalabani,na uponyaji huo hupokelewa kwa ombi la imani. (Isa.53:1-5;Mk.16:16-18).

**G.** Katika ubatizo wa Roho Mtakatifu pamoja na ushuhuda wa kunena kwa lugha kunakofua - tana na Tunda la Roho, kunakopokelewa kwa imani ikiambatana na masharti ya Biblia ya kupokea ubatizo huo. (Yoh.7:37;14:16-17;16:12-15;Mdo.1:8;2:1-4;10:44-47;19:2-6).

**H.** Kanisa ni watu walioitwa na Mungu kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kutoka ulimwenguni na kuwekwa wakfu kwa ajili yake, kwa kuzaliwa mara ya pili na kuunganishwa katika mwili wa Kristo, ambaye ni kichwa cha Kanisa. Kazi ya Kanisa ni kumpenda na kumtukuza Mungu na kuhubiri Injili kwa kila kiumbe na kuishi katika tumaini la ufufuo wa wafu.(Mt.5:13-14;Yoh.15:1,2;Mdo.1:8;Efe.1:7,22;4:11-16;5:23;2 Kor. 6:6-18).

## IBARA YA 7: TUNU ZA KANISA

Tunathamini uhai na utu wa binadamu;tunathamini na kuheshimu ibada;tunathamini uadilifu katika kila tufanyalo;tunathamini uaminifu kwa Biblia kama Neno la Mungu,tunathamini Kanisa ;tunathamini ndoa na familia,tunathamini maishayenye ushuhuda mwema na utakatifu; tunathamini kuhubiri Injili iliyojaa nguvu za Roho Mtakatifu; tunathamini ubora katika kila tufanyalo;tunathamini haki;tunathamini amani, tunathamini
umoja na mshikamano;tunathamini upendo na utulivu.

## IBARA YA 8: MAAGIZO MAKUU

Maagizo yafuatayo yamekubalika kufuatwa na washirika wa Kanisa la Pentecostal Assemblies of God (Tanzania).

**A.** Kila Mshirika wa Kanisa la Pentecostal Assemblies of God (Tanzania) awe amezaliwa mara ya pili na kubatizwa katika maji mengi. (Mt. 28:19, Rum. 6:4).

**B.** Kila Mshirika wa Kanisa la **PAG (T)** atashiriki Meza ya Bwana (Ushirika Mtakatifu) ambayo ni Mkate na Divai,kinywaji kisichokuwa na kilevi ili kulinda ushirika wake na Mungu na Washirika wengine na kuendelea kutangaza kifo cha Bwana wetu Yesu Kristo msalabani, Ufufuo wake na Tumaini la Kurudi kwake. (Mk.14:22-24,1Kor. 11:26).

## IBARA YA 9: USHIRIKA

Kanisa la Pentecostal Assemblies of God (Tanzania) litakuwa na waumini wa aina mbili.

**A.** **Mfuasi:**

Mfuasi ni mtu aliyejiunga na Kanisa la Pentecostal Assemblies of God (Tanzania) lakini hajatimiza sifa za Ushirika.

**B.** **Mshirika:**

Mshirika ni Mfuasi aliyetimiza sifa za Ushirika wa Kanisa la Pentecostal Assemblies of God (Tanzania) na kupokelewa rasmi kwa kupewa mkono wa Ushirika.

**C.** **Sifa za Mshirika:**

1. Amempokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yake.

2. Ikiwa ameoa au kuolewa, lazima awe na ndoa iliyo halali au amebariki ndoa yake kama Ibara ya 42 inavyofafanua.
3. Awe amejifunza Kanuni ya Imani na Ushirika na kukubali kutimiza mafundisho yote.
4. Awe amebatizwa katika maji mengi na kuenenda katika Roho Mtakatifu.

**D. Haki za Mshirika:**

1. Kupokelewa rasmi katika Kanisa.
2. Kupokea huduma ya Neno la Mungu toka kwa Mchungaji.
3. Kutembelewa na Mchungaji.
4. Kushiriki katika shughuli za Kanisa.
5. Kupokea Meza ya Bwana.
6. Kustahili kuchagua au kuchaguliwa kuwa kiongozi.
7. Kupokea cheti cha Ubatizo.
8. Anaweza kupangiwa kuhubiri au kufundisha akiwa ana uwezo.
9. Anapohama au anaposafiri anatakiwa apewe baruaya utambulisho kwenda kwenye Kanisa anakohamia.

**E. Wajibu wa Mshirika:**

1. Kuishi maisha matakatifu.
2. Kuleta wengine kwa Yesu Kristo.
3. Kuheshimu na kustahi Mchungaji na viongozi wengine wa Kanisa.
4. Kuhudhuria kwa uaminifu ibada za Kanisa.
5. Kutoa sadaka na fungu la kumi kanisani kwa uaminifu.
6. Kuchangia maendeleo ya Kanisa.
7. Kutenga Jumapili kwa ajili ya kumwabudu Mungu.
8. Kufanya ibada ya familia kila siku kama inavyowezekana.
9. Kupiga kura katika mikutano ya Kanisa ambayo yeye ni mjumbe.

**F. Ukomo wa Ushirika:**

1. Kuacha imani ya **PAG (T).**
2. Asipotimiza masharti ya Kanuni ya Imani ya Kanisa la **PAG (T).**
3. Anapolihama Kanisa la **PAG (T)**.
4. Asipohudhuria ibada za kanisani bila taarifa kwa kipindi kinachozidi miezi sita.
5. Mshirika au kiongozi yeyote anapoacha ushirika au ushirika wake unapokoma,

haruhusiwi kuchukua mali yoyote ya **PAG (T).**

**G. Mshirika anayehamia toka makanisa mengine:**

Anaweza kupokelewa kuwa Mshirika wa **PAG (T)** kwa utaratibu ufuatao:

1. Kama akija na barua toka kwa Mchungaji alikotoka; akiwa kiongozi apate barua ya kiongozi aliye juu yake.
2. Akubaliane na Kanuni ya Imani ya Kanisa la **PAG (T).**
3. Endapo itashindikana kuja na barua, Mchungaji wa Kanisa atampokea kama Mfuasi mpaka atakapotimiza sifa ya Mshirika.

**H. Marudio:**

Iwapo mshirika atapatikana na kosa, aweza kuwekwa chini ya marudio kufuatana na Kanuni ya Imani ya Ushirika ya **PAG (T).**

## SURA YA 2: USIMAMIZI WA MALI ZA KANISA

## IBARA YA 10: WADHAMINI WA KANISA

### A. Idadi ya Wadhamini:

Kutakuwa na Baraza la wadhamini la **PAG (T)** ambalo litaitwa **"THE REGISTERED TRUSTEES OF THE PENTECOSTAL ASSEMBLIES OF GOD (TANZANIA)"**lenye wajumbe wasiopungua 7 au wasiozidi 9 ambao watasajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### B. Kuundwa kwa Baraza la Wadhamini:

1. Halmashauri Kuu ya Pentecostal Assemblies of God (Tanzania) itateua wajumbe watakaounda Baraza la Wadhamini, na uteuzi huo utathibitishwa na Mkutano Mkuu.
2. Endapo upungufu wa idadi ya wajumbe utajitokeza kabla ya kipindi cha Baraza kuisha,Halmashauri Kuu inaweza kuteua jina au majina mengine ya wajumbe kujaza pengo hilo na uteuzi huo utatangazwa kwenye Muhtasari wa Halmashauri Kuu.
3. Askofu Mkuu na Katibu Mkuu watakuwa ni wajumbe wa Baraza la Wadhamini isipokuwa hawatashika nafasi ya Mwenyekiti na Katibu. Mwenyekiti atateuliwa na Halmashauri Kuu na

Katibu wa Baraza la Wadhamini atateuliwa kutokana na wajumbe wa Baraza katika Mkutano wa kwanza chini ya usimamizi wa Askofu Mkuu.

4. Baraza litaundwa kwa kuzingatia jiografia ili kurahisisha utendaji.

**C. Wajibu na mamlaka ya Wadhamini:**

Wadhamini watakuwa na mamlaka kamili ya udhamini bila kuathiri masharti ya dhamana waliyokabidhiwa.

1. Watasimamia umilikaji wa mali zote za **PAG (T)** zinazohamishika na zisizohamishika kwa uangalifu na uaminifu kwa niaba ya Kanisa la Pentecostal Assemblies of God (Tanzania).
2. Watatoa ushauri kwa mipango ya mikopo yenye tija, upangishaji majengo au viwanja, uhamishaji wa mali, na matumizi mengine ya ardhi ili kuleta ufanisi katika kuiendeleza **PAG (T).**
3. Watahakiki na kuhifadhi nyaraka halisi za mali ya Kanisa la **PAG (T).**

4. Watatunza na kuthibiti matumizi ya Muhuri wa Baraza la Wadhamini.
5. Ofisi ya Baraza la wadhamini itakuwa katika ofisi za makao makuu ya Kanisa la **PAG (T)**.

**D. Kipindi cha Udhamini:**

1. Muda wa udhamini utakuwa kipindi cha miaka mitano na aweza kuchaguliwa tena.
2. Kila baada ya miaka mitano Wadhamini watapitishwa upya na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu.

**E. Sifa za mjumbe wa Baraza la Wadhamini:**

1. Awe ni mwanamume au mwanamke mkristo thabiti, Mtanzania, aliyeokoka na kushika imani ya Kanisa la **PAG (T)**,aliye tayari kuunga mkono malengo, madhumuni, na mikakati ya Kanisa la Pentecostal Assemblies of God (Tanzania).
2. Awe Mchungaji au Mtumishi aliyesimikwa mwenye umri usiopungua miaka 40 au kuzidi 70,na awe mshirika wa **PAG(T)** kwa miaka isiyopungua kumi.
3. Awe anajua kusoma na kuandika katika lugha zote mbili ya Kiswahili na Kiingereza

na elimu yake ya chini iwe ni kiwango cha diploma.

4. Awe mtu mwadilifu asiyekuwa na tamaa ya mali, mwenye bidii katika kazi ili kuleta ufanisi katika dhamana aliyokabidhiwa.
5. Awe mtu mwenye umakini,jasiri,na mwenye utayari wa kukubaliana au kutokubaliana kwa hoja.

**F. Mikutano ya Baraza la Wadhamini:**

1. Baraza la Wadhamini litakutana mara mbili kwa mwaka isipokuwa kama kuna dharura mwenyekiti aweza kuitisha kikao.
2. Agenda za Mkutano zitatangazwa kwa kipindi cha miezi mitatu kabla, isipokuwa mkutano wa dharura.
3. Mkutano halali lazima uwe na idadi ya theluthi mbili ya wajumbe.
4. Endapo Mwenyekiti ameitisha kikao na akawa na dharura Baraza laweza kukaa chini ya Mwenyekiti wa muda atakayechaguliwa na wajumbe chini ya Katibu wa Baraza la Wadhamini.
5. Bajeti ya Vikao vya Baraza la Wadhamini itapitishwa na Halmashauri Kuu.

**G. Ukomo wakuwa Mjumbe wa Baraza la Wadhamini:**

Udhamini wa mjumbe wa Barazala Wadhamini waweza kufikia kikomo endapo:

1. Iwapo hatachaguliwa.
2. Atafariki,atachanganyikiwa,au kuishiwa uwezo wa kufanya kazi.
3. Ataihama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi kinachozidi mwaka mmoja.
4. Atajiuzulu kwa maandishi na kujiuzulu kwake kuridhiwa na Halmashauri Kuu na taarifa kutolewa kwenye Mkutano Mkuu.
5. Akianguka dhambini,kuasi imani,au kulihama Kanisa la Pentecostal Assemblies of God (Tanzania).
6. Atahukumiwa na mahakama, hukumu itakayoathiri sifa za kuwa Mdhamini isipokuwa itakapothibitika kuwa hukumu inatokana na kutetea Imani ya Kikristo.
7. Kutohudhuria vikao viwili vya kawaida bila taarifa.
8. Ataacha kuwa Mshirika wa Kanisa la Mahali (Local Church).

**H. Muhuri wa Wadhamini:**

1. Utakuwa wa moto (seal) wenye maneno **"THE REGISTERED TRUSTEES OF THE PENTECOSTAL ASSEMBLIES OF GOD (TANZANIA)".**
2. Utatumika sio chini ya Wadhamini wawili.
3. Muhuri huo utatunzwa katika ofisi ya Wadhamini.

## SURA YA 3: MIKUTANO, MABARAZA NA KAMATI

### IBARA YA 11: MKUTANO MKUU

**A.** Mkutano Mkuu ndio ngazi ya juu kabisa katika Uongozi wa Kanisa la **PAG (T)**.

**B.** Wajumbe wa Mkutano Mkuu watakuwa ni Wachungaji wote waliosimikwa na ambao hawajasimikwa pamoja na wenzi wao wa ndoa,Walimu wote na wenzi wa ndoa wanaofundisha katika shule za Biblia na vyuo vya Biblia ambao ni washirika wa Kanisa la PAG (T),Wakurugenzi wa Idara mbalimbali hadi ngazi ya wilaya, Wamisionari wakazi,na Viongozi wote ngazi ya Taifa,Jimbo,na Wilaya na wenzi wao wa ndoa.

**C.** Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu atakuwa ni Askofu Mkuu.

**D.** Mkutano Mkuu wa uchaguzi utaitishwa na Halmashauri Kuu mara moja kila baada ya miaka mitano mahali itakapopanga.

**E.** Halmashauri Kuu yaweza kuitisha Mkutano Mkuu wa dharura endapo kutakuwa na jambo maalumu linalotakiwa kufanyiwa maamuzi na Mkutano Mkuu.

**F.** Mkutano Mkuu wa uchaguzi utapiga kura kuwachagua Askofu Mkuu,Makamu Askofu Mkuu,Katibu Mkuu,Naibu Katibu Mkuu Wajumbe Wawili,na Wakurugenzi wa Idara mbalimbali katika ngazi ya Taifa (kila idara italeta majina matatu ili kupigiwa kura).

**G.** Utapokea Neno na Mafundisho toka kwa wahubiri na walimu waliopangwa na Halmashauri kuu.

**H.** Kutakuwa na akidi ya asilimia hamsini (50%) ya wajumbe wote wa Mkutano mkuu waliohudhuria.

**I.** Mkutano Mkuu utatangazwa kwa muda usiopungua miezi mitatu.

**J.** Mkutano Mkuu utapokea taarifa ya kazi kutoka kwa viongozi.

**K.** Msimamizi wa Mkutano Mkuu wa uchaguzi atateuliwa na Halmashauri Kuu.

## IBARA YA 12: HALMASHAURI KUU

**A.** Hii itakuwa kamati ya ngazi ya juu kiutendaji katika Kanisa la **PAG (T)**.

**B.** Halmashauri kuu itaundwa na Askofu. Mkuu, Makamu Askofu Mkuu,Katibu Mkuu,Naibu Katibu Mkuu,Maaskofu wa Majimbo,

Wajumbe wawili waliochaguliwa na Mkutano Mkuu na Wakurugezi wa Idara mbalimbali za **PAG (T)** kitaifa.

**C.** Askofu Mkuu ndiye atakayekuwa Mwenyekiti wa vikao vyote vya Halmashauri Kuu isipokuwa atakapokuwa anajadiliwa.

**D.** Halmashauri Kuu itakutana mara tatu kwa mwaka ila yaweza kukutana zaidi inapobidi.

**E.** Itapokea ripoti kutoka majimboni na kuzijadili agenda zilizowasilishwa.

**F.** Itakuwa na uwezo wa kuunda kamati ndogo ndogo ili kutekeleza majukumu mbalimbali ya dharura.

**G.** Itaandaa Mkutano Mkuu wa**PAG (T)** kitaifa.

**H.** Itaidhinisha Wachungaji watakaowekewa mikono.

**I.** Itawaombea leseni za kufungisha ndoa toka serikalini Wachungaji wenye sifa za kufungisha ndoa.

**J.** Itaweka mipango ya pesa na kusimamia pesa zote kwa kazi zote za **PAG (T)**.

**K.** Kutafuta na kusimamia mchakato wa kupata vibali vya kufanya kazi hapa nchini

watumishi wanaotoka nje ya Tanzania ili kufanya kazi na **PAG (T)**.

**L.** Itapitisha Majimbo na Wilaya mpya zilizokidhi viegezo.

**M.** Itasimamia kazi ya **PAG (T)** kwa ujumla na kutoa taarifa kwa Mkutano mkuu.

**N.** Mwisho wa kukaa madarakani kwa Halmashauri Kuu utakuwa ni miezi sitini au miaka mitano.

**O.** Itahakikisha Baraza la Wadhamini linalinda na kuhakiki mali za **PAG(T)**.

**P.** Itasimamia kazi za Idara mbalimbali na Taasisi nyingine za **PAG (T)**.

**Q.** Itasimamia nidhamu ya Viongozi na Wachungaji.

**R.** Itapanga bajeti ya Halmashauri Kuu, Baraza la Wadhamini,na Mkutano mkuu.

**S.** Itasimamia wajibu na haki za Wachungaji na Viongozi.

**T.** Itatatua migogoro mbalimbali inayotokea katika Kanisa la **PAG (T)** hasa ya Kitaifa au yaweza kuunda kamati maalumu ya usuluhishi.

**U.** Kutakuwa na Kamati tendaji ambayo wajumbe ni Askofu Mkuu, Makamu Askofu Mkuu,Katibu Mkuu,Naibu Katibu Mkuu.

i) Watakutana kila mara inapohitajika.

ii) Ndiyo itakayosimamia Maadili ya viongozi kwa niaba ya Halmashauri Kuu.

iii) Itapanga na kukisia gharama ya uendeshaji wa Makao makuu na shughuli zake kwa ujumla.

iv) Itasimamia kazi na kutathimini taarifa zote za maendeleo ya utekelezaji wake kama zilivyopendekezwa na Halmashauri kuu ya **PAG (T)**.

v) Kusimamia maamuzi ya Halmashauri Kuu ya **PAG (T)**.

vi) Itakuwa na uwezo wa kutatua matatizo ya dharura yanayojitokeza na kupeleka taarifa katika kamati ya Halmashauri Kuu.

## IBARA YA 13: BARAZA LA WAANGALIZI

**A. Wajumbe wa Baraza la Waangalizi.**

1. Wajumbe wote wa Halmashauri Kuu.
2. Waangalizi wote wa Wilaya.
3. Wajumbe wa Baraza la Wadhamini.
4. Maaskofu wakuu wastaafu.

**B. Vikao na kazi za Baraza la Waangalizi.**

1. Mwenyekiti wa vikao vyote vya Baraza atakuwa Askofu Mkuu.
2. Litakutana mara moja kwa mwaka.
3. Laweza kukutana zaidi ya mara moja kama halmashauri Kuu ya **PAG (T)** itakavyoamua.
4. Taarifa ya kikao itatolewa sio chini ya siku tisini.
5. Wajumbe watapokea mafunzo maalumu toka kwa walimu walioandaliwa na Halmashauri Kuu ya **PAG (T)**.
6. Wajumbe watapokea taarifa ya kazi ya Mungu kutokangazi ya Taifa, Majimbo na Idara ngazi ya Taifa.
7. Baraza litajadili taarifa hizo na kutoa maoni jinsi ya kuboresha kazi ili kuleta ufanisi.

8. Baraza litapendekeza majina ya wagombea kwa mkutano Mkuu wa Uchaguzi **PAG (T)** ili yapigiwe kura na wajumbe.
9. Baraza watapitia Rasimu ya mabadiliko ya Katiba na kutoa mapendekezo yao ambayo yatapelekwa kwa Mkutano Mkuu baada ya kuhakikiwa na Halmashauri Kuu ya **PAG (T)**.

## IBARA YA 14: JIMBO

### A. Sifa za kuwa Jimbo.

1. Jimbo litaundwa kwa kibali cha Halmashauri Kuu.
2. Litakuwa na Wilaya zisizopungua tatu.
3. Mipaka ya Kijiografia ya Jimbo itategemea ilivyokubalika na Halmashauri za Wilaya zilizomo katika Jimbo, Halmashauri ya Jimbo husika,na kupitishwa na Halmashauri Kuu.
4. Litakuwa na wachungaji wasiopungua kumi na tano waliowekewa mikono.
5. Litakuwa na ofisi ya Jimbo.
6. Litakuwa na uwezo wa kujiendesha, na kuchangia mapato ya ofisi ya Askofu Mkuu.

**B. Mkutano Mkuu wa Jimbo.**

1. Utakutana mara moja kila baada ya miaka mitano.
2. Utafanyika jimboni baada ya Mkutano Mkuu wa Taifa.
3. Msimamizi wa Mkutano Mkuu wa uchaguzi wa jimbo atakuwa ni Askofu Mkuu au mjumbe kutoka Halmashauri kuu aliyeteuliwa na Askofu Mkuu.
4. Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa jimbo watakuwa wachungaji wote wasimikwa na ambao hawajasimikwa pamoja na wenzi wao wa ndoa, viongozi wote wa idara kuanzia ngazi ya wilaya.
5. Utatangazwa kwa muda usiopungua siku tisini.
6. Utapokea na kujadili taarifa ya Kazi ya Mungu toka kwa viongozi.
7. Utapokea taarifa ya fedha na taarifa za idara mbalimbali.
8. Utapiga kura kumchagua Askofu wa Jimbo, Makamu Askofu wa Jimbo, Katibu wa Jimbo, Naibu Katibu wa Jimbo,

wajumbe wawili, na wakurugenzi wa Idara.

9. Majina ya Wagombea Jimboni yatapendekezwa na Wachungaji wote wasimikwa wanaotambuliwa na Halmashauri Kuu na kupelekwa kwa Mkutano mkuu wa Jimbo.
10. Mwenyekiti wa Mkutano huu atakuwa Askofu wa Jimbo.
11. Utapokea mafundisho toka kwa walimu waliopangwa na Halmashauri ya Jimbo.
12. Halmashauri ya Jimbo yaweza kuitisha Mkutano wa Jimbo wa dharura.

**C. Halmashauri ya Jimbo.**

1. Wajumbe wake ni Askofu wa Jimbo,Maka mu Askofu wa Jimbo,Katibu wa Jimbo,Nai bu Katibu wa Jimbo,Waangalizi wa wilaya, wajumbe wawili,na wakurugenzi wa idara mbalimbali ngazi ya Jimbo.
2. Itakutana mara tatu kwa mwaka au zaidi inapobidi.
3. Itapokea taarifa za kazi kutoka kila Wilaya.
4. Itajadili mambo yanayohusu kazi ya Mungu katika Jimbo.

5. Itasimamia mipango yote ya pesa Jimboni pasipo kuathiri mipango ya Halmashauri Kuu.
6. Itaandaa Mkutano Mkuu wa Jimbo.
7. Itapanga bajeti ya kila mwaka ya kuendesha kazi ya Mungu Jimboni.
8. Itatatua migogoro mbalimbali katika Jimbo au kuunda kamati maalumu ya usuluhishi.
9. Kutakuwa na Kamati tendaji.
   - i) Itakutana mara kwa mara ikibidi.
   - ii) Wajumbe wake ni Askofu wa Jimbo, Makamu Askofu wa Jimbo,Katibu wa Jimbo na Naibu Katibu wa Jimbo.
   - iii) Watasimamia utekelezaji wa mipango na maazimio ya Halmashauri ya Jimbo.
   - iv) Wataandaa gharama za uendeshaji wa mipango na maazimio ya Halmashauri ya Jimbo.
   - v) Watatatua matatizo yanayojitokeza ghafla na kupeleka ripoti kwa Halmashauri ya Jimbo.

## IBARA YA 15: WILAYA

### A. Sifa za kuwa Wilaya.

1. Wilaya itaundwa chini ya kibali cha Halmashauri Kuu baada ya kukamilika kwa mchakato wa kuunda Wilaya.
2. Iwe na Makanisa yasiyopungua kumi.
3. Iwe na Wachungaji waliowekewa mikono wasiopungua watano.
4. Iwe na uwezo wa kujiendesha kimapato.
5. Iwe na uwezo wa kuchangia maendeleo ya Jimbo.
6. Mipaka ya kijiografia ya Wilaya itategemea ilivyokubalika na Halmashauri ya Wilaya na Halmashauri ya Jimbo husika na kupitishwa na Halmashauri Kuu.
7. Iwe na ofisi ya Wilaya.

### B. Mkutano Mkuu wa Wilaya.

1. Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa Wilaya atakuwa ni Mwangalizi wa wilaya.
2. Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya watakuwa ni Wachungaji wote waliosimikwa na wasiosimikwa pamoja na wenzi wao wa ndoa,na wakurugenzi wote wa Idara mbalimbali wa Wilaya,Assembli na Kanisa la mahali.

3. Utafanyika kila baada ya miaka mitano na utachagua viongozi wa Wilaya.
4. Halmashauri ya Wilaya yaweza kuitisha Mkutano wa dharura wa Wilaya.
5. Utapokea mafundisho na mahubiri toka kwa wahudumu walioandaliwa.
6. Utapokea taarifa ya kazi ya Mungu Wilayani na kutoa mapendekezo ya kuboresha kazi ya Mungu.
7. Msimamizi wa uchaguzi atakuwa ni Askofu wa Jimbo au mjumbe yeyote wa Halmashauri ya Jimbo aliyeteuliwa na Askofu wa Jimbo.

**C. Halmashauri ya Wilaya.**

1. Halmashauri ya wilaya itaundwa na Mwangalizi wa wilaya, Makamu Mwangali-zi wa wilaya,Katibu wa Wilaya,Naibu Katibu wa Wilaya,Waangalizi wa Assembli ,wajumbe wawili, na wakurugenzi wa idara mbalimbali wa wilaya.
2. Mwenyekiti atakuwa ni Mwangalizi wa Wilaya.
3. Itakutana mara tatu kwa mwaka au zaidi ikibidi.

4. Itapokea taarifa ya kazi kutoka kwa Waaangalizi wa Assembli.
5. Itajadili maswala yote yanayohusu kazi ya Mungu Wilayani.
6. Itapanga bajeti ya kila mwaka ya uendeshaji wa kazi ya Mungu wilayani.
7. Itaandaa Mkutano Mkuu wa Wilaya.
8. Yaweza kutoa mapendekezo ya uhamisho wa Mchungaji Jimboni,lakini haina mam-laka ya kumhamisha Mchungaji aliyesimi-kwa bila idhini ya Halmashauri Kuu.
9. Itasuluhisha migogoro au kuunda kamati maalumu ya usuluhishi.
10. Kamati tendaji.

    i) Itakutana mara kwa mara ikibidi.
    ii) Wajumbe wake ni Mwangalizi wa wilaya,Makamu Mwangalizi wa Wilaya,Katibu wa wilaya na Naibu Katibu wa Wilaya.
    iii) Watasimamia utekelezaji wa mipango na maazimio ya Halmasha -uri ya Wilaya.

iv) Wataandaa gharama za uendeshaji wa mipango na Halmashauri ya Wilaya.

v) Watatatua matatizo yanayojitokeza ghafla na kupeleka ripoti kwa Halmashauri ya Wilaya.

**D. Baraza la Wachungaji la Wilaya.**

1. Baraza hili litaundwa na Wachungaji wasimikwa na wasiosimikwa pamoja na wenzi wao wa ndoa .
2. Mwenyekiti atakuwa ni Mwangalizi wa Wilaya.
3. Litakutana mara mbili kwa mwaka au zaidi ikibidi.
4. Baraza hili litakuwa na lengo kuu la kudumisha ushirika wa kiroho wa Wachungaji.
5. Litafanya maombi ya pamoja kwa njia linaloona inafaa.
6. Litapendekeza majina ya watakaopigiwa kura na Mkutano Mkuu wa Wilaya.

## IBARA YA 16: KAMATI YA ASSEMBLI

### A. Sifa za kamati ya Assembli.

1. Kamati ya Assembli ni wachungaji wa makanisa jirani yaliyoko katika eneo moja.
2. Halmashauri ya Wilaya itasimamia utaratibu wa kuweka mipaka ya Assembli.

### B. Wajumbe wake.

1. Wachungaji wote wa makanisa yaliyoko kwenye Assembli waliosimikwa na wasiosimikwa.
2. Viongozi wa idara mbalimbali wa Assembli.

### C. Kazi zake.

1. Kuendeleza na kudumisha ushirika wa Wachungaji ili kuimarisha makanisa.
2. Kujenga huduma ya masaidiano kati ya Wajumbe.
3. Utakutana kila mwezi ila waweza kukutana mara nyingi zaidi.
4. Kuweka mpango wa kusaidiana wakati wote.
5. Watakapokutana katika mkutano wao chini ya Mwangalizi wa wilaya watamcha-gua Mwenyekiti,Katibu,Mtunza hazina na Watia saini katika Hati za fedha.

6. Watabadilishana Uongozi kila baada ya miaka mitano.

**D. Kamati Tendaji ya Assembli.**

1. Wajumbe wake ni Mwangalizi, Katibu na Mhasibu.
2. Kutekeleza maamuzi ya kamati ya Assembli.
3. Kushughulikia mambo ya dharura ya Assembli.
4. Itawajibika kwa Kamati ya Assembli.

## IBARA YA 17: KANISA LA MAHALI

**A. Muundo wa Kanisa la Mahali.**

1. Huu ni mkusanyiko wa Washirika wa mahali pamoja chini ya Mchungaji Kiongozi.
2. Washirika hawa hukutana katika ibada za jumapili na ibada za katikati ya wiki na katika mikutano mingine kadiri inavyopa - ngwa na Kanisa hilo.
3. Kanisa la mahali litakuwa na Wazee wa Kanisa kwa idadi inayotegemea ukubwa wa Kanisa.
4. Kamati ya Kanisa itakuwa na wajumbe wafuatao:Mchungaji, Mzee au Wazee,

Katibu,Mtunza hazina,na Viongozi wa Idara mbalimbali.

5. Mke wa Mchungaji au Mume wa Mchungaji aweza kuwa mjumbe kamati ya Kanisa akiwa Mshirika.

**B. Kazi za Kamati ya Kanisa.**

1. Kupanga shughuli za maendeleo ya Kanisa la mahali.
2. Kusimamia mipango ya Kanisa chini ya Mchungaji kiongozi.
3. Kutoa huduma za kiroho na kijamii kwa Washirika wa Kanisa na jamii iliyolizunguka Kanisa.
4. Kusimamia na kutunza pesa na mali nyinginezo za Kanisa.
5. Kuchagua watia sahihi kwenye akaunti za benki.
6. Kusuluhisha migogoro au kuunda kamati maalumu ya usuluhishi inapobidi.

**C. Jinsi ya kuwapata viongozi wa Kanisa la mahali.**

1. Kwa kuwa Uchungaji ni wito Mchungaji hatapigiwa kura.

2. Uongozi wa juu kwa Uongozi wa Roho Mtakatifu waweza kumtuma Mchungaji katika Kanisa la mahali.
3. Mchungaji atateua Viongozi wa Kanisa na Mkutano Mkuu wa Kanisa utawadhibitisha.
4. Sifa za Mshirika lazima zizingatiwe katika kuwapata Viongozi.

**D. Kuondolewa kwa mjumbe katika Kamati ya Kanisa.**

1. Pale atakapokwenda kinyume na masharti na sifa za Mshirika.
2. Mjumbe mwingine yeyote wa kamati ya Kanisa aweza kuondolewa na Mchungaji kiongozi akishirikiana na Kamati ya Kanisa baada ya makosa ya mjumbe huyo kuthibitika kwa zaidi ya mashahidi wawili waaminifu.

**E. Wajibu wa Kanisa la Mahali.**

1. Kushiriki katika mipango inayopangwa na Uongozi wa ngazi za juu wa Kanisa la **PAG (T)**.
2. Kufungua makanisa mapya na kuyalea.

3. Kupanga mipango ya maendeleo na kuanzisha miradi mbalimbali ya Kanisa.
4. Kutafuta mali za Kanisa,kuzilinda, na kuziendeleza.
5. Kupokea wafuasi wapya na kuwasaidia kutimiza masharti ya Washirika wa **PAG (T)**.
6. Kutunza Mchungaji/Wachungaji wake.
7. Kujenga uwezo wa kujitegemea kwa njia ya kukusanya sadaka, fungu la kumi,na michango mingine.
8. Kuandaa Viongozi wapya na kuwaendeleza.

## SURA YA 4: VIONGOZI WA KANISA LA PAG (T)

### IBARA YA 18: ASKOFU MKUU

**A. Sifa za Askofu Mkuu.**

1. Awe mwenye sifa zilizotajwa katika Biblia. (ITimotheo 3:1-7;Tito.1:7-9,na I Petro 5:2-3).
2. Awe mwenye umri kuanzia miaka arobaini hadi sabini (40-70)
3. Awe amesoma shule ya Biblia.
4. Awe Mchungaji msimikwa aliyetumikia Kanisa la **PAG (T)**. kwa kipindi kisichopungua miaka kumi (10).
5. Awe mchungaji wa Kanisa la mahali.
6. Awe na uwezo wa kuongoza.
7. Awe raia wa Tanzania.

**B. Kazi za Askofu Mkuu.**

1. Atakuwa ndiye mwidhinishaji wa matumizi ya fedha za Halmashauri Kuu.
2. Atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu, Halmashauri Kuu na Baraza la Waangalizi isipokuwa katika Mkutano Mkuu wa Uchaguzi na katika kamati ambazo zinamjadili.

3. Atatia sahihi kwenye vyeti na vitambulisho vya Wachungaji.
4. Atakuwa Mwangalizi wa masuala yote yana yohusu Kanisa kwa ujumla.
5. Atalinda Katiba ya **PAG (T)**.
6. Atakuwa ndiye Mwakilishi na Msemaji mkuu wa Kanisa katika mialiko ya sherehe na mikutano mbalimbali ya kiroho na kiserikali ndani na nje ya Tanzania.
7. Atasimamia Uchaguzi Mkuu wa Majimbo.
8. Atakuwa mjumbe katika Baraza la Wadhamini.
9. Atakuwa ndiye Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la **PAG (T)**.
10. Atafundisha Wachungaji.
11. Atapewa majukumu ya utekelezaji kama itakavyopangwa na Halmashauri Kuu katika Sera na Mpango Mkakati wa Kanisa.

**C. Kuondolewa kwake madarakani.**

1. Askofu Mkuu atasimamishwa uongozi kwa kura za siri za maandishi kwa theluthi mbili (2/3) za wajumbe wa kamati ya Halmashauri Kuu ya **PAG (T)**,akienda kinyume na Kanuni ya Imani na Ushirika na Katiba ya **PAG (T)**.

2. Akijiuzulu mwenyewe.
3. Akianguka dhambini au kwenda kinyume na sifa zake katika (1Timotheo3;1-7, Tito 1:7-9,IPetro 5:2-3).
4. Ikibainika kwamba kuendelea kuongoza kwake kutaleta vurugu, migongano na kuondoa umoja wa Kanisa la **PAG (T)** na baada ya juhudi za kumsaidia kushindikana.
5. Baada ya Halmashauri Kuu ya **PAG (T)** kumsimamisha, Mkutano Mkuu wa dharura utaitishwa ili kuthibitisha uamuzi huo.
6. Mkutano Mkuu utapewa nafasi ya kumsikiliza na kufanya maamuzi ya mwisho juu ya Askofu Mkuu huyo.
7. Baada ya Askofu Mkuu kusimamishwa,taarifa ya Mkutano Mkuu wa dharura itatolewe sio chini ya siku tisini.
8. Ikiwa Mkutano Mkuu utaridhika na hatua iliyochukuliwa na Halmashauri Kuu,basi Uchaguzi Mkuu utafanyika kwenye Mkutano huohuo ili kumpata Askofu Mkuu mwingine.

**D. Uwajibikaji wake.**

Askofu Mkuu atawajibika kwa Halmashauri Kuu na kwa Mkutano Mkuu wa **PAG (T)**.

## IBARA YA 19: MAKAMU ASKOFU MKUU

**A. Sifa za Makamu Askofu mkuu.**

Awe na sifa sawa na Askofu Mkuu.

**B. Kazi zake.**

1. Atakaimu kazi zote za Askofu Mkuu, iwapo kuna hali yoyote itakayomfanya Askofu Mkuu asiweze kutekeleza kazi zake.
2. Atakaimu kazi zote kwa muda wa siku tisini iwapo Askofu Mkuu atajiuzulu ghafla,akifariki au kusimamishwa uongozi.
3. Atapewa majukumu ya utekelezaji kama itakavyopangwa na Halmashauri Kuu ya **PAG (T)** na Askofu mkuu.
4. Atakuwa mweka saini wa kwanza katika Hati za fedha za Halmashauri kuu.

**C. Kuondolewa kwake madarakani.**

Ataondolewa madarakani na Halmashauri Kuu kwa sababu zilezile za Askofu mkuu na mwingine atateuliwa na Halmashauri kuu.

**D. Uwajibikaji wake.**

Makamu wa Askofu Mkuu atawajibika kwa Askofu Mkuu na kwa Halmashauri Kuu.

## IBARA YA 20: KATIBU MKUU

### A. Sifa zake.

1. Awe mwenye sifa zilizotajwa katika Biblia.(1Timotheo 3:1-7;Tito 1:7-9;na 1Petro 5:2-3).
2. Awe mwenye umri kuanzia miaka arobaini hadi sabini (40-70)
3. Awe amemaliza shule ya Biblia.
4. Awe ni Mtumishi Msimikwa au Mchungaji Msimikwa kwa kipindi kisichopungua miaka kumi.

### B. Kazi zake.

1. Atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa **PAG (T)**.
2. Ataandaa na kuitisha Mikutano ya Halmashauri Kuu, Baraza la Waangalizi na Mkutano Mkuu kwa idhini ya Askofu Mkuu.
3. Atatayarisha taarifa ya Halmashauri Kuu itakayowakilishwa kwenye Mkutano Mkuu na Askofu Mkuu.
4. Atakuwa mweka saini wa pili katika hati za fedha za **PAG (T)**.

5. Atatia saini kwenye vyeti na vitambulisho vyote vya Wachungaji.
6. Ataandaa,atasambaza,na kuweka kumbukumbu Mihtasari ya vikao na kumbukumbu nyinginezo za kitaifa.
7. Atasimamia shughuli za mipango na fedha, mawasiliano, idara za maendeleo na ustawi wa jamii,idara ya elimu,idara ya umisheni,na watumishi wote katika ofisi ya **PAG (T)** taifa.
8. Atawakilisha taarifa ya fedha katika Mkutano Mkuu.

**C. Kuondolewa kwake madarakani.**

1. Ataondolewa na Halmashauri Kuu, kutokana na sababu zile zile zinazomsimamisha Askofu Mkuu na Makamu Askofu Mkuu.
2. Akisimamishwa Makamu atashika nafasi yake na taarifa itatolewa katika Mkutano Mkuu.
3. Anaweza kujiuzulu kwa maandishi endapo kuna sababu zinazomfanya asiweze kutimiza majukumu yake.

**D. Uwajibikaji wake.**

Katibu Mkuu atawajibika kwa Askofu Mkuu na kwa Halmashauri Kuu.

## IBARA YA 21: NAIBU KATIBU MKUU

**A. Sifa zake.**

Atakuwa na sifa sawa na zile za Katibu Mkuu.

**B. Kazi zake.**

1. Atashika kazi zote za Katibu mkuu endapo hayupo.
2. Mweka saini wa tatu katika Hati za fedha za Halmasahauri kuu.
3. Atafanya kazi atakazopewa na Katibu mkuu.

**C. Atawajibika.**

Kwa Katibu Mkuu, Askofu mkuu na Halmashauri Kuu.

**D. Kuondolewakwake madarakani.**

Ataondolewa madarakani na Halmashauri Kuu kwa sababu zilezile zinazomwondoa Katibu Mkuuna mwingine atawekwa na Halmashauri kuu.

## IBARA YA 22: ASKOFU WA JIMBO

### A. Sifa zake.

1. Awe mwenye sifa zilizotajwa katika Biblia.(1Timotheo 3:1-7;Tito 1:7-9; na 1Petro 5:2-3).
2. Awe mwenye umri kuanzia miaka thelathini na tano hadi sabini (35-70).
3. Awe amesoma shule ya Biblia**.**
4. Awe Mchungaji msimikwa kwa kipindi kisichopungua miaka kumi.
5. Awe Mchungaji wa Kanisa la mahali.

### A. Kazi zake.

1. Atakuwa mwidhinishaji wa matumizi ya fedha za Halmashauri ya Jimbo.
2. Atakuwa Mwenyekiti wa mikutano ya Jimbo na mkutano wa viongozi wa dharura, isipokuwa katika Mkutano Mkuu wa uchaguzi na mikutano ambayo anajadiliwa.
3. Atasimamia Mkutano wa Uchaguzi wa Wilaya.
4. Atakuwa Msimamizi Mkuu katika Jimbo.

**B. Kuondolewa kwake.**

1. Askofu wa Jimbo atasimamishwa na Halmashauri Kuu baada ya taarifa zake kuwasilishwa na Jimbo.
2. Uamuzi wa kumsimamisha Askofu wa Jimbo kabla ya muda wake wa uongozi kuisha lazima ufikiwe kwa uamuzi wa theluthi mbili (2/3) ya kura za wajumbe wa Halmashauri kuu.
3. Sababu za kusimamishwa au kuondolewa madarakani ni kuwa kinyume na sifa zake (1Tim.3:1-7).
4. Kupokea maoni kutoka Halmashauri ya Jimbo lake na kubainika kuwa kuongoza kwake kutaleta vurugu na baada ya jitihada za kumsaidia kushindikana.
5. Akianguka dhambini au kwenda kinyume na sifa zake katika 1Timotheo 3;1-7,Tito 1:7-9 na 1Petro 5:2-3.
6. Akijiuzulu mwenyewe kwa maandishi na sababu za kujiuzulu zikaridhiwa na Halmashauri ya Jimbo.
7. Baada ya hapo Mkutano wa Jimbo utaitishwa na Halmashauri kuu ili kuthibiti-

sha uamuzi huo na mwingine atachaguliwa kwenye mkutano huo.

**C. Atawajibikaji kwa.**

1. Halmashauri ya Jimbo.
2. Halmashauri Kuu.
3. Mkutano Mkuu wa Jimbo.
4. Askofu Mkuu.

## IBARA YA 23: MAKAMU ASKOFU WA JIMBO

**A. Sifa zake.**

Ni sawa na za Askofu wa Jimbo.

**B. Kazi zake.**

1. Atakaimu kazi zote za Askofu wa Jimbo iwapo hayupo,ikiwa amejiuzulu ghafla, akiwa amesimamishwa au akifariki.
2. Atakaimu kazi hiyo kwa muda utakaowekwa na Halmshauri Kuu.
3. Atakuwa mweka saini wa kwanza katika Hati za fedha.

**C. Kuondolewa kwake madarakani.**

1. Ataondolewa madarakani na Halmashauri ya Jimbo kwa sababu zile zile za kumuondoa Askofu wa Jimbo.

2. Atakapoondolewa, Makamu Askofu wa Jimbo mwingine atateuliwa na Halmashauri ya Jimbo.

**D. Kuwajibika kwake.**

1. Atawajibika kwa Askofu wa Jimbo.
2. Atawajibika kwaHalmashauri ya Jimbo.

**IBARA YA 24: KATIBU WA JIMBO**

**A. Sifa zake.**

1. Awe mwenye sifa zilizotajwa katika Biblia. (1Timotheo 3:1-7;Tito1:7-9,naPetro 5:2-3).
2. Awe mwenye umri kuanzia miaka thelathini hadi sabini (30-70).
3. Awe amesoma shule ya Biblia.
4. Awe ni Mchungaji Msimikwa kwa kipindi kisichopungua miaka mitano.

**B. Kazi zake.**

1. Atasimamia Mapato na Matumizi ya pesa za Jimbo.
2. Atamsimamia mhasibu wa kuajiriwa au kujitolea aliyewekwa na Halmashauri ya Jimbo.
3. Ataandaa mihtasari ya mikutano na vikao vyote vya Jimbo.

4. Atatunza kumbukumbu za wachungaji na makanisa katika Jimbo.
5. Ataandaa taarifa itakayowakilishwa na Askofu wa Jimbo katika Mkutano wa Jimbo.
6. Atawakilisha taarifa ya fedha katika Mkutano wa Jimbo.
7. Atakuwa mweka saini wa pili katika Hati za fedha.

**C. Kusimamishwa na Kuondolewa kwake madarakani.**

1. Katibu wa Jimbo atasimamishwa na Halmashauri ya Jimbo na taarifa zake kupelekwa kwa Halmashauri Kuu.
2. Halmashauri kuu ikiridhika na sababu zilizomsimamisha itamwondoa madarakani.
3. Uamuzi wa kumsimamisha Katibu wa Jimbo kabla ya muda wake wa uongozi kuisha lazima ufikiwe kwa uamuzi wa theluthi mbili (2/3) ya kura za wajumbe.
4. Sababu za kusimamishwa au kuondolewa madarakani ni kuwa kinyume na sifa zake (1 Tim. 3:1-7).
5. Kupokea maoni kutoka Halmashauri ya Jimbo lake na kubainika kuwa kuongoza

kwake kunakiuka Katiba na kuhatarisha utulivu katika Jimbo baada ya jitihada za kumsaidia kushindikana.

6. Baada ya kusimamishwa Makamu Katibu wa Jimbo atakaimu nafasi ya Katibu wa Jimbo.

**D. Katibu wa Jimbo atawajibika.**

1. Kwa Askofu wa Jimbo.
2. Kwa Halmashauri ya Jimbo.
3. Kwa Halmashauri Kuu.
4. Kwa Mkutano Mkuu wa Jimbo.

## IBARA YA 25: NAIBU KATIBU WA JIMBO

**A. Sifa zake.**

Sawa na sifa za Katibu wa Jimbo.

**B. Kazi zake.**

1. Atakaimu kazi zote za Katibu wa Jimbo wakati hayupo.
2. Atakuwa mweka saini wa tatu katika Hati za fedha.

**C. Kuondolewa kwake madarakani.**

Sababu za kumwondoa madarakani ni sawa na sababu zinazomwondoa madarakani Katibu wa Jimbo na Halmashauri ya Jimbo itamteua mwingine kujaza nafasi yake.

**D. Kuwajibika.**

Makamu Katibu atawajibika kwa Katibu wa Jimbo, Askofu wa Jimbo na Halmashauri ya Jimbo.

**IBARA YA 26: MWANGALIZI WA WILAYA**

**A. Sifa zake.**

1. Sifa zake ziwe sawa kama zilivyotajwa katika Biblia.
   (1Timotheo 3:1-7.Tito 1:7-9,1Petro 5:2-3).
2. Awe ametumikia PAG (T) kwa muda usiopungua miaka saba (7).
3. Awe Mchungaji msimikwa.
4. Awe amesoma shule ya Biblia.
5. Awe mwenye umri wa miaka ishirini na tano hadi sabini. (25-70)
6. Awe Mchungaji wa Kanisa la mahali.

**B. Kazi zake.**

1. Atakuwa Mwangalizi wa kazi kwa ujumla katika Wilaya.
2. Atakuwa Mwidhinishaji wa Matumizi ya Hati za fedha za Wilaya.
3. Atakuwa Mwenyekiti wa Mikutano yote ya Wilaya, isipokuwa katika vikao vile ambavyo

anajadiliwa pia katika Mkutano mkuu wa Wilaya wa Uchaguzi.

**C. Kusimamishwa na Kuondolewa kwake madarakani.**

1. Atasimamishwa na Halmashauri ya Jimbo kwakura za siri za maandishi ya thelufhi mbili (2/3) na taarifa kupelekwa kwa Halmashauri ya Kuu na mwingine kuwekwa badala yake kwa siku tisini kisha uchaguzi ufanyike.
2. Sababu za kuondolewa kwake ni kujiuzulu mwenyewe,kifo, kuanguka dhambini,kuwa kinyume na sifa zake.
3. Ikiwa kamati ya Jimbo imepokea maoni toka Halmashauri ya Wilaya na jitihada ya kumsaidia kushindikana.

**D. Atawajibika kwa.**

1. Halmashauri ya Jimbo.
2. Halmashauri ya Wilaya.
3. Mkutano Mkuu wa Wilaya.

**IBARA YA 27: MAKAMU MWANGALIZI WA WILAYA**

**A. Sifazake.**

Ni sawa na zile za Mwangalizi wa Wilaya.

**B. Kazi yake.**

1. Kukaimu kazi zote za Mwangalizi wa Wilaya ikiwa kuna jambo au hali yoyote inayomfanya Mwangalizi asitekeleze wajibu wake.
2. Atakuwa mtia saini wa kwanza katika vitabu vya fedha vya Wilaya.

**C. Atawajibika.**

Kwa Mwangalizi wa Wilaya na Halmashauri ya Wilaya.

**D. Ataondolewa.**

Na Halmashauri ya Wilaya kwa theluthi mbili (2/3) ya kura na mwingine kuwekwa na Halmashauri ya wilaya.

## IBARA YA 28: KATIBU WA WILAYA.

**A. Sifa zake.**

Ni sawa na zile za Mwangalizi wa Wilaya.

**B. Kazi zake.**

1. Ni mtia saini wa pili katika vitabu vya fedha vya Wilaya.
2. Atasimamia ukusanyaji na uwakilishaji wa pesa za Wilaya toka makanisani kwenda wilayani na Jimboni.

3. Atamsimamia Mhasibu aliyeteuliwa au kuajiriwa na Wilaya.
4. Atatayarisha mihtasari ya vikao vya mikutano ya Wilaya.
5. Atakuwa mtekelezaji wa kazi atakazopewa na mwangalizi wa Wilaya au Halmashauri ya Wilaya.

**C. Atawajibika kwa.**

1. Mwangalizi wa Wilaya.
2. Halmashauri ya Wilaya.
3. Mkutano Mkuu wa Wilaya.

**D. Kusimamishwa na kuondolewa madarakani.**

1. Aweza kusimamishwa na Halmashauri ya wilaya kwa theluthi mbili (2/3) ya kura za siri za wajumbe.
2. Kwa kukosa maadili mema,kufariki,kujiuzulu kuanguka dhambini,kuwa kinyume na sifa zake.
3. Baada ya taarifa zake kupelekwa Jimboni najuhudi za kumsaidia kushindikana.
4. Makamu wake atakaimu nafasi hiyo.

## IBARA YA 29: NAIBU KATIBU WA WILAYA.

**A. Sifa zake.**

Ni sawa na sifa za Mwangalizi wa Wilaya**.**

**B. Kazi zake.**

1. Atafanya kazi zote kama atakavyoagizwa na katibu wa Wilaya.
2. Atakaimu majukumu ya Katibu wakati hayupo.
3. Atakuwa mweka saini wa tatu katika vitabu vya fedha za Wilaya.

**C. Kuwajibika kwake.**

1. Kwa Mwangalizi wa Wilaya.
2. Kwa Halmashauri ya Wilaya.
3. Kwa Katibu wa Wilaya.

**D. Kusimamishwa na kuondolewa madarakani.**

1. Atasimamishwa na kuondolewa madarakani na Halmashauri ya wilaya .
2. Atasimamishwa na kuondolewa madarakani kwa sababu zilezile zinazomwondoa Katibu wa Wilaya na mwingine atawekwana Halmashauri ya wilaya.

## IBARA YA 30: MWANGALIZI WA ASSEMBLI

### A. Sifa zake.

1. Awe na sifa za (1Timotheo 3:1-7).
2. Awe ni Mchungaji Msimikwa na anayechunga kanisa.
3. Awe ameongoza kanisa siyo chini ya miaka mitano.
4. Awe na umri wa miaka 20-70.
5. Awe amesoma shule ya Biblia.

### B. Kazi zake.

1. Mwenyekiti wa Kamati ya Assembli isipokuwa anapojadiliwa.
2. Msimamizi wa kazi zote katika Assembli.
3. Atasimamia chaguzi za Kanisa.
4. Atakuwa mjumbe katika kamati ya Wilaya.
5. Mwidhinishaji wa matumizi ya fedha za Assembli.

### C. Kuwajibika.

1. Atawajibika kwa Halmashauri ya Assembli na Halmashauri ya Wilaya.

### D. Kuondolewa.

1. Akikosa sifa ya (1Timotheo 3:1-7).

2. Ataondolewa kwa kura ya 2/3 ya wajumbe wa Assembli na kuthibitishwana Halmashauri ya Wilaya.

## IBARA YA 31: KATIBU WA ASSEMBLI

**A. Sifa zake.**

Awe na sifa zile zile za Mwangalizi wa Assembli.

**B. Kazi zake.**

1. Ataandaa mihtasari ya vikao vya Assembli.
2. Mtendaji wa kazi atakazopewa na mwangalizi wa Assembli.

**C. Atawajibika**kwa Mwangalizi wa Assembli na kamati ya Assembli.

**D. Ataondolewa na** Kamati ya Assemblikwa kukosa sifa.

## IBARA YA 32: MCHUNGAJI WA KANISA LA MAHALI

**A. Sifa zake.**

1. Amezaliwa mara ya pili na amebatizwa kwa maji mengi.
2. Amebatizwa na Roho Mtakatifu na kunena kwa lugha.
3. Awe na wito wa kumtumikia Mungu.

4. Awe amesoma shule ya Biblia.
5. Ikiwa ameanzisha Kanisa kabla ya kujiunga na shule ya Biblia, atatakiwa ajiunge na masomo, afanye hivyo bila kuchelewa.
6. Awe na sifa zilizoainishwa kwenye (1Tim 3:1-7 Tito 1:7-9, 1Petro5:2-3).
7. Baada ya kutimiza masharti husika mchungaji atawekewa mikono na kuitwa mchungaji Msimikwa.
8. Awe na umri usiopungua miaka kumi na nane (18).

**B. Kazi za Mchungaji wa Kanisa la Mahali.**

1. Ni mwenyeketi wa vikao vyote vya Kanisa isipokuwa pale ambapo anajadiliwa, Mwangalizi wa Assembli atakuwa ni Mwenyekiti.
2. Ndiye Msimamizi mkuu wa shughuli za maendeleo ya Kanisa.
3. Ni mshauri wa idara zote za Kanisa.
4. Ni Mwidhinishaji mkuu wa fedha za Kanisa.
5. Ndiye atakayependekeza majina ya viongozi wa Kanisa la mahali kwa mkutano Mkuu wa Kanisa ili kuthibitishwa na mkutano huo.
6. Mchungaji aweza kuliongoza Kanisa kulingana na wito wake.

**C. Atawajibika kwa.**

1. Kanisa lake na Assembli.
2. Halmashauri ya Wilaya.
3. Halmashauri ya Jimbo.
4. Halmashauri Kuu.

**D. Kusimamishwa na kuondolewa kw Mchungaji.**

1. Kamati ya Kanisa haina mamlaka ya kumwondoa Mchungaji kiongozi.
2. Makosa ya Mchungaji yaweza kutolewa taarifa na kamati ya Kanisa na Assembli na kuthibitishwa na Halmashauri ya Wilaya kwa ushahidi wa maandishi na kupigiwa kura ya maandishi ya theluthi mbili (2/3) ya wajumbe wa kamati husika.
3. Aweza kusimamishwa na Jimbo na kuondolewa kazini na Halmashauri kuu.
4. Makosa yanayoweza kumwondoa Mchungaji ni kwenda kinyume cha Katiba ya **PAG (T)** na kukosa sifa za Kichungaji (1Tim 3:1-7).
5. Adhabu nyingine mbadala yaweza kutolewa na Halmashauri ya Jimbo na taarifa kupelekwa kwa Halmashauri Kuu.

## IBARA YA 33: KATIBU WA KANISA

**A. Sifa Zake.**

1. Awe mwaminifu.
2. Mtu anayejua kutunza siri za Kanisa.
3. Awe na elimu ya kumwezesha kufanya kazi ya Katibu kulingana na hali ya Kanisa.
4. Awe ni Mshirika mwaminifu, yaani mwenye kutimiza wajibu wake kama Mshirika.
5. Atathibitishwa na Mkutano mkuu wa Kanisa la mahali kati ya majina yatakayopendekezwa na Mchungaji kiongozi.

**B. Kazi zake.**

1. Atahusika na maandalizi ya ripoti ya Kanisa ambayo itawakilishwa kwenye kamati la Kanisa.
2. Ataandika na kutunza mihtasari ya vikao vya Kanisa.
3. Atafanya kazi nyinginezo kama atakavyoagizwa na Mchungaji kiongozi.

**C. Atawajibika**kwa Mchungaji na kamati ya kanisa.

**D. Ataondolewa**na Mchungaji na Kamati ya Kanisa na mwingine ateuliwe wa badala yake.

## SURA YA 5: MAMBO MBALIMBALI YA KANISA

### IBARA YA 34: KUPIGA KURA

**A.** Kura zote katika vikao na Mikutano ya Kanisa la **PAG (T)** zitakuwa za siri na kwa maandishi.

**B. Jinsi ya kupata wagombea.**

1. Ngazi ya taifa majina yatapendekezwa na Baraza la Waangalizi.
2. Baraza la Waangalizi litateua majina sita miongoni mwao, watakaosimamia uteuzi wa majina ya wagombea kwa kura ya siri, nao pia watapiga kura na miongoni mwao anaweza kuteuliwa kugombea nafasi yoyote.
3. Baraza la Waangalizi litateua majina sita ya mwanzo kulingana na wingi wa kura ambazo kila aliyependekezwa amepata.
4. Hao watu sita watakaoteuliwa watapewa muda kusimama na kusalimia Baraza la Waangalizi.
5. Majina sita yatapigiwa kura tena yapatikane majina matatu yatakayopelekwa moja kwa moja kwenye Mkutano Mkuu.
6. Wale watatu walioteuliwa watapewa nafasi ya kusimama na kujitambulisha majina yao mbele ya Mkutano Mkuu.

7. Baada ya kujieleza mbele ya Mkutano Mkuu watapigiwa kura za siri kwa maandishi.
8. Kiongozi atapatikana kwa theluthi mbili (2/3) ya kura zote zilizopigwa,lakini utaratibu wa theluthi mbili (2/3), ukishindikana mara tatu itachukuliwa kura ya kuzidi.
9. Kwa ngazi ya Jimbo na Wilaya utafuata utaratibu huo hapo juu. Isipokuwa kwenye ngazi ya Jimbo majina ya wagombea yatapendekezwa na Wachungaji wasimikwa wanaotambuliwa na Halmashauri Kuu. Katika ngazi ya Wilaya majina ya wagombea yatapendekezwa na Wachungaji wasimikwa na wasiowasimikwa wanaotambuliwa na Jimbo.

## IBARA YA 35: IDARA ZA PAG (T)

**A.** Halmashauri Kuu ya **PAG (T)** itaunda Idara za Kanisa la **PAG (T)** ngazi ya Taifa, kwa madhumuni maalumu ya **PAG (T)**.Kanisa la mahali laweza kuunda Idara nyingine kulingana na mahitaji ya Kanisa.

**B.** Kwa sasa **PAG (T)** itakuwa na Idara zifuatazo ambazo zitakuwa na miongozo yake:

1. Idara ya Elimu na Mafunzo.

2. Idara ya Wanawake ambayo kwa kifupi ni WWK.
3. Idara ya Vijana ambayo kwa kifupi itaitwa CA.
4. Idara ya Umisheni na Uinjilisti.
5. Idara ya Watoto.
6. Idara ya Wanaume.

**IBARA YA 36: HUDUMA ZA JAMII**

**A.** Huduma za Hifadhi ya jamii.

Kanisa la **PAG (T)** litajihusisha na huduma za hifadhi ya jamii kama kuendesha vituo vya watoto yatima, wazee,huduma za afya kama vile Hospitali, Zahanati na Vituo vya afya.

**B.** Huduma za Maendeleo.Hizi zitakuwa ni huduma kama vile shule za awali,shule za msingi, sekondari, vyuo,vyuo vikuu,shughuli za ujasiriamali ,kilimo,uvuvi,taasisi za fedha, utunzaji wa mazingira, na stadi nyingine kwa viongozi, washirika wake na jamii inayowazunguka.

**IBARA YA 37: KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA KIOFISI.**

Zifuatazo zitaingizwa katika kumbukumbu na Nyaraka za kiofisi za Kanisa la Pentecostal Assemblies of God (Tanzania).

A. Katiba ya Pentecostal Assemblies of God (Tanzania).

B. Hati za Usajili wa Kanisa.

C. Hati ya Usajili wa Wadhamini.

D. Muhuri wa Baraza la Wadhamini wenye kuandikwa maneno **"The Registered Trustees of the Pentecostal Assemblies of God (Tanzania**)".

E. Kumbukumbu ya mali toka Baraza la Wadhamini na Mikataba muhimu.

F. Muhuri wa Askofu Mkuu.

G. Muhuri wa Katibu mkuu ambao utakuwa ukiidhinisha kazi zote zilizoainishwa kuwa kazi za Katibu Mkuu.

H. Sheria ndogo ndogo, Kanuni ya Imani na Ushirika, na Mihtasari yote ya Halmashauri Kuu na Mkutano Mkuu na taarifa za majimbo na Idara za Kitaifa.

I. Tovuti ya Kanisa la **PAG (T)**na mitandao mingine ambako **PAG (T)** ina akaunti.

J. Kumbukumbu za Matukio muhimu.

K. Certificate of Registration for Taxpayer Identification Number (TIN).

## IBARA YA 38: UHUSIANO WA PAG (T) NA MASHIRIKA MENGINE

A. **PAG (T)** itashirikiana na mashirika mengine yale yenye malengo yanayofanana.

B. Mahusiano hayo yatakuwa ya hiari na yasiyofu-ngamana na upande wowote.

C. Kanisa la mahali (Local Church) au Idara itakuwa huru kushirikiana na mtu yeyote au shirika lolote kwenye shughuli za kujiletea maendeleo bila kuathiri imani au Katiba ya **PAG (T)** na taarifa zake zipelekwe kwa Halmashauri Kuu.

## IBARA YA 39: MAWASILIANO

**PAG (T)** itaendesha vyombo vya mawasiliano kama vile Redio, Television, Magazeti, na Mitandao ya kijamii ikizingatia maadili, na bila kuathiri imani na Katiba ya **PAG (T)**.

## IBARA YA 40: UTARATIBU WA KUTATUA MIGOGORO

**A.** Migogoro yoyote ndani ya Kanisa la **PAG (T)** itasuluhishwa ndani ya Kanisa la **PAG (T)** katika ngazi husika.

**B.** Endapo mgogoro utashindikana kutatuliwa katika ngazi husika utapelekwa kwa ngazi iliyo juu yake na kama ngazi zote zitashindwa utapelekwa kwenye vyombo vingine vya usuluhishi kwa ajili ya utatuzi kwa mujibu wa (Mathayo 18:15-17.)

## IBARA YA 41: UTUMISHI

**A. Aina za Watumishi**

1. Kanisa la **PAG (T)** litakuwa na watumishi wahubiri,ambao ni Wachungaji,Walimu, Wainjilisti, Manabii, na Wamisionari

   (Waf. 4:11-12).

2. Watumishi waajiriwa.

3. Watumishi wa kujitolea.

**B. Haki za Mtumishi**

1. Halmashauri kuu itatengeneza Sheria ndogo ndogo za utumishi wa Kanisa.

2. Watumishi waajiriwa haki zao zitazingatia mikataba yao ya kazi.
3. Makanisa yawawekee wachungaji akiba ya uzeeni katika mifuko ya hifadhi ya jamii.

**C. Wajibu wa Watumishi**

1. Wajibu wa kila mtumishi utazingatia mkataba wake wa kazi.
2. Kuheshimu Katiba ya **PAG (T)**.

## IBARA YA 42: NDOA

**A.** Kanisa la **PAG (T)** linakubali ndoa kati ya mwanamume mmoja na mwanamke mmoja na kifo ndicho kitakacho watenganisha.(Mat. 19:1-6).

**B.** Ndoa zisizokuwa za Kikristo na zinazokubalika kisheria na kibiblia zitahitaji kubarikiwa mtu anapokuwa mshirika wa **PAG (T)**.

## IBARA YA 43: MAPATO NA MATUMIZI YA PESA

**A. Njia za mapato**

1. Sadaka .2. Zaka (Fungu la kumi). 3. Michango.
4. Wafadhili naMiradi.

**B. Matumizi**

Matumizi ya pesa yatazingatia taratibu zilizopo katika ngazi na idara husika kama inavyoelekezwa na Halmashauri kuu.

**IBARA YA 44: SHERIA NDOGO NDOGO**

**A.** Mikutano na vikao vyote vya Kanisa la **PAG (T)** vyaweza kutengeneza taratibu za amri na mikataba katika vikao; ila amri hizo na mikataba hiyo isiwe kinyume na Maandiko Matakatifu, Katiba ya **PAG(T),** na Kanuni ya Imani na Ushirika.

**B.** Sheria ndogo ndogo ambazo zitatungwa na Baraza lolote lazima zithibitishwe na ngazi iliyoko juu yake.

**IBARA YA 45: MAREKEBISHO YA KATIBA**

**A.** Marekebisho ya Katiba ya **PA (T)** yaweza kufikiriwa kufanyika kutoka katika Halmashauri Kuu,Halmashauri ya Jimbo,na Halmashauri ya wilaya.

**B.** Marekebisho hayo yakishatayarishwa na Halmashauri Kuu ndipoyatapelekwa katika Baraza la Waangalizi kisha Mkutano Mkuu na kupitishwa kwa kura ya theluthi mbili (2/3) ya wajumbe waliohudhuriana kupelekwa Wizarani kwa Msajili kwa hatua za mwisho.

**KATIBA YA PAG (T) YA MWAKA 2017.**

**KANUNI CHINI YA IBARA YA 44.**

**UTANGULIZI**

Pentecostal Assemblies of God (T) ni kanisa lenye Imani ya Kipentekoste. Kanisa hili linaendesha shughuli zake kwa kufuata Neno la Mungu, Katiba na Sheria ndogo ndogo (kanuni), ambayo iko katika Sura ya 5 Ibara ya 44.

**SEHEMU YA KWANZA: UFAFANUZI WA IBARA ZA KATIBA.**

**Sura ya 2 - Ibara ya 10 B (1).**

Mkutano mkuu utawathibitisha Wadhamini waliopendekezwa na Halmashauri kuu kwa njia ya kusema ndiyo au hapana, endapo utata ukitokea watu wanyoshe mikono na kuhesabiwa.

**Sura ya 2 - Ibara ya 10 E (1) na G (8).**

Sifa za mjumbe: Mwanamke Mtumishi aweza kuwa Mdhamini.

Mjumbe wa Baraza la Wadhimini atakoma kuwa Mdhamini akikoma kuwa mshirika wa PAG (T).

**Sura ya 3 - Ibara ya 11 (F).**

Kamati ya Idara husika itapendekeza majina matatu ya wagombea ngazi ya taifa na kuyaleta mbele ya Baraza la Waangalizi na baada ya kujadiliwa na yakikubalika yataenda mbele ya Mkutano mkuu ili yapigiwe kura.

**Sura ya 3- Ibara ya 11 (i).**

Mkutano Mkuu utatangazwa na Halmashauri kuu kupitia miniti za Halmashauri kuu kama njia kuu kwa muda usiopungua miezi mitatu au siku tisini, na utaratibu huu utatumika kwa ngazi ya jimbo na wilaya.

**Sura ya 3 - Ibara ya 14 A (4), B (4).**

Kwa mujibu wa Ibara ya 14 A (4), na B (4), “Kuwekewa mikono” ni Kusimikwa mchungaji kwa kazi maalumu.

**Sura ya 3- Ibara ya 15 (B) 2.**

Katika Katiba hii Ibara 15 (B), 2; neno Wenzi”
linamaanisha mke au mume Mshirika.

**Sura ya 3 - Ibara ya 15 (B) 7.**

Askofu wa Jimbo aliyeko madarakani ndiye atakayesimamia chaguzi za wilaya zilizoko jimboni mwake na atasimikwa siku ya pili baada ya uchaguzi. Na mtiririko huu ndiyo utafuatwa toka ngazi ya Taifa hadi wilaya.

**Sura ya 3 -Ibara ya 17 (c) (3,4).**

1. Mchungaji atateua Wazee, Mashemasi, Viongozi wa Idara, Katibu na Mhasibu miongoni mwa washirika wa kanisa na kuthibitishwa na Mkutano mkuu wa kanisa.
2. Na endapo kutakuwa na nafasi za wazi, Mchungaji anaweza kuteua kwa kujaza nafasi na kuthibitishwa na Baraza la wazee.
3. Sifa zao zitakuwa sawa na (1Timotheo 3:8-13, Matendo 6:3-6).
4. Kamati ya Kanisa ni Mchungaji, Wazee, na Viongozi wa Idara za Kanisa.
5. Kumsaidia/Kumshauri Mchungaji katika kuliongoza kanisa ili kufikia ufanisi.
6. Wazee wanaweza kuendesha ibada ya mazishi kwa maelekezo ya Mchungaji.
7. Kamati/Wazee wa kanisa hawana mamlaka ya kumuwajibisha Mchungaji.
8. Muda wa wazee kukaa madarakani ni miaka miwili (2)lakini Mchungajiaweza kufanya mabadiliko akisha uriana na kamati ya Kanisa.
9. Mzee wa kanisa ataondolewa kwenye nafasi yake na Mchungaji kwa kushirikisha kamati ya Kanisa.
10. Mzee wa kanisa atawajibika kwa Mchungaji na kwa Kamati ya Kanisa.

**Sura ya 4 - Ibara ya 32 a (7).**

**SIFA ZA KUSIMIKWA KWA MCHUNGAJI**

1. Awe amezaliwa mara ya pili.
2. Amebatizwa kwa maji mengi.
3. Amepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.
4. Awe na ushuhuda mwema katika nyumba yake na watu wengine.
5. Awe amemaliza masomo ya shule ya Biblia.
6. Awe ameongoza Kanisa au huduma kwa muda wa miaka miwili.
7. Awe na ndoa ya Kikristo.
8. Mtumishi anayetoka dhehebu lingine.
   a) Achunguzwe na kupimwa na kamati husika.
   b) Kamati hiyo yaweza kupendekeza asome katika Chuo cha Biblia.

**Sura ya 4 - Ibara ya 32 B.**

Huduma ya Mchungaji msimikwa na Mchungaji ambaye hajasimikwa;

1. Mchungaji Msimikwa atafanya huduma zote za kichungaji kama vile kutoa Meza ya Bwana, kubatiza, kuweka watoto wakfu, kuendesha ibada ya mazishi,isipokuwa kufungisha ndoa ambayo itabidi kuombewa leseni serikalini.

2. Mchungaji ambaye hajasimikwa atafanya huduma zote za kiuchungaji isipokuwa kufungisha ndoa, meza ya Bwana, kubatiza na kubariki watoto.
3. Kwa viongozi wanaohitajika kuidhinishwa/kuthibitish-wa na Mkutano au kikao kura ya wazi ya Ndiyo au Hapana itatumika na endapo utata utajitokeza watanyoosha mikono na kuhesabiwa.

**Sura ya 5 -Ibara ya 34 (B).**

1. Uteuzi wa majina ya wagombea utafanyika siku hiyohiyo ya Mkutano Mkuu wa uchaguzi.
2. Hairuhusiwi kupiga kampeni katika chaguzi za kanisa.
3. Endapo itatokea miongoni mwa wale sita, atateuliwa kugombea nafasi yoyote ni lazima ataachia nafasi ya usimamizi na mwingine ateuliwe.
4. Nafasi ya Askofu Mkuu: Majina matatu yatapendekezwa kwa ajili ya nafasi ya Askofu Mkuu katika Mkutano Mkuu. Kama ilivyo kwa Askofu Mkuu ndivyo itakuwa kwa Makamu Askofu Mkuu.
5. Nafasi ya Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu itafuata utaratibu uliotumika kwa nafasi ya Askofu Mkuu na Makamu wake.

6. Utaratibu huu utafanyika kwenye kuwapata Wajumbe wa Mkutano Mkuu, na Kamati za Idara zitateua watatu na kuleta mbele ya Baraza la Waangalizi.

**Sura ya 5- Ibara ya 35 (B).**

Kila kamati ya idara itaandaa Mwongozo wake wa utendaji kazi na mwongozo huo ni lazima uidhinishwe na Halmashauri Kuu.

**Sura ya 5- Ibara ya 36 (A-B).**

Kanisa la PAG (T) litaendesha huduma za jamii kwa ngazi zote za kanisa na kila ngazi itakuwa na ukaguzi wake, kuanzia Taifa hadi Kanisa la mahali pamoja.

**Sura ya 2 - Ibara ya 10 (C), 3,4; na Sura ya 2 Ibara ya 37 (A-K).**

Kumbukumbu, nyaraka, na hati halisi za mali zitatunzwa katika Kabati maalumu Makao makuu chini ya uangalizi wa Wadhamini.

**Sura ya 5- Ibara ya 38 ya (A-C).**

Ngazi zote za Kanisa zinaruhusiwa kuwa na mahusiano na Mashirika mengine au mtu kwa kujiletea maendeleo.

**Sura ya 5- Ibara ya 39 (A).**

Kanisa la PAG (T) katika ngazi zote na idara zake zaweza kuanzisha vyombo vya mawasiliano kwa kuzingatia Katiba na vitakuwa chini ya Halmashauri kuu.

**Sura ya 5- Ibara ya 41 (B). HAKI ZA WATUMISHI.**

Ijapo utumishi huu niwakujitolea, lakini watumishi hawa watakuwa na haki zifuatazo.

1. Posho za watumishi wote wa PAG(T) zitapangwa na ofisi ile wanayotumika, isipokuwa kwa Wachungaji kamati ya kanisa yaweza kutumia utaratibu wa asilimia sabini (70%) au kumpangia Mchungaji posho ya kila mwezi.
2. Mtumishi ambaye ni Mchungaji, atasimikwa kwa ajili ya huduma.
3. Mtumishi atapata Kitambulisho pale anapotumika.
4. Mtumishi anatakiwa kujiunga na Mfuko wa huduma.
5. Mtumishi ataingizwa kwenye mifuko ya huduma za jamii sawa na taratibu za ofisi anayotumika.
6. Kanisa laweza kumjengea mtumishi nyumba binafsi kununuliwa usafiri nakusaidiwa watoto kupata elimu na misaada mengineyo kwa kadri ya uwezo wa Kanisa analoongoza.

7. Wagane na wajane wa watumishi waweza kusaidiwa kwa jinsi ofisi itakavyoona ni vema.
8. Watoto yatima ambao wazazi wao walikuwa watumishi waweza kusaidiwa kutegemeana na uwezo wa ofisi ambayo wazazi wao walikuwa wanatumika.
9. Mtumishi anaposimikwa atapata hati ya Ukiri, Kusimikwa (Certificate of Ordination) kwenye nafasi aliyochaguliwa.
10. Mtumishi ambaye amechaguliwa anapomaliza utumishi wake kwenye nafasi ile akiwa amepiga vita vizuri na kuilinda imani atatunukiwa cheti cha Shukra ni kwa utumishi wake (Award/Certificate of Appreciation).

**Sura ya 5 -Ibara ya 42.**

1. Mchungaji anaweza kufungisha ndoa kama amepata Leseni ya usajili wa ndoa kutoka Serikalini.
2. Mshirika au Kiongozi wa kanisa la PAG (T) haruhusiwi kuoa au kuolewa na mtu mwenye imani tofauti na imani ya Kipentekoste.
3. Mwanaume ambaye ana mke zaidi ya mmoja, atabakia kanisani kama mfuasi na mke halali ni yule wa kwanza, na wake zake wengine watakuwa wafuasi.

4. Kanisa la PAG (T) haliruhusu ndoa ya jinsia moja.
5. Msajili wa ndoa atatakiwa kufuata taratibu za Serikali wakati wa kufungisha ndoa.
6. Ndoa itasimamiwa na wadhamini (Mashahidi) ambao ni Mme na Mke wake ambaye ndoa yao ina ushuhuda mzuri na wawe wanatoka kanisa la kipentekoste.
7. Mwanamume na mwanamke wanaokusudia kuoana washauriwe kupima afya.
8. Taratibu zote za ndoa na sherehe zitazingatia Maadili ya kikristo.
9. Mafundisho ya ndoa kwa wanaokusudia kuoana yapewe muda wa kutosha.
10. Taratibu za Mahari ni jambo linalohusu wazazi lakini lizingatie Maadili yakikristo.

**Sura ya 5 - Ibara ya 43 (a) (b).**

1. Mwaka wa Fedha wa kanisa la PAG (T) utaanza Januari hadi Desemba.
2. Kila Kiongozi, Mshirika, na Mfuasi anawajibika kutoa Sadaka na Fungu la kumi la mapato yake yote kwa uaminifu, mapato yanayotokana Fedha, Mazao, Mifugo na mengineyo.

3. Wale ambao sio waaminifu katika ulipaji wa mafungu ya kumi watachukuliwa hatua na kamati husika.
4. Kutakuwa na Mtunza fedha kwa ngazi zote za uongozi wa PAG (T), na atahakikisha kwamba anatunza kumbukumbu zote za fedha, sawa na taratibu za fedha na zitakuwa wazi kwa kukaguliwa/ukaguzi.
5. Katika ngazi ya Taifa, Jimbo na Wilaya fedha zote zitawekwa benki, ila katika ngazi ya Asembli/Kanisa ikiwezekana.
6. Kiongozi yeyote hana mamlaka ya kutumia fedha au kukaa na fedha bila idhini ya kamati husika.
7. Sadaka na Mafungu ya kumi zitahesabiwa kila zinapotolewa na watu wasiopungua wawili na kuwekwa kumbukumbu kabla ya kuwasilishwa kwa Mhasibu.
8. Mtunza fedha katika ngazi yeyote atatoa migawo, na posho za watumishi kwa wakati itakavyowezakana.
9. Kila ngazi inawajibika kutoa taarifa ya fedha (mapato na matumizi) kama ilivyopangwa na kamati husika.
10. Sadaka ya malimbuko, shukrani na nadhiri ni ya mchungaji haitaingizwa kwenye migawo ya kanisa isipokuwa pale ambapo kuna maelekezo mengine.
11. Ngazi yeyote ya uongozi haina mamlaka ya kukopa kwenye taasisi bila kibali cha Baraza la Wadhamini.

**Sura ya 5- Ibara ya 44.**
Sheria ndogo ndogo maana yake ni Kanuni.

**Sura ya 5 - Ibara ya 45.**
Baada ya Mkutano Mkuu kupitisha Marekebisho ya Katiba yatapelekwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Msajili wa Vyama kwa ajili kusajiliwa hapo ndipo yataanza kutumika pamoja Sheria ndogo ndogo.

**SEHEMU YA PILI: MENGINEYO.**

1. Shule ya Biblia/Chuo cha Biblia ambayo Mchungaji wakanisa la PAG (T) anatakiwa asome ni ile inayotambuliwa na Halmashauri kuu.
2. Kiongozi wa ngazi ya juu anaweza kuingia kwenye kamati zilizoko chini yake ikilazimu kwa ajili ya kuleta ufanisi wa kazi.
3. Mchungaji kiongozi aweza kuteua Mchungaji msaidizi baada ya kujadiliana na baraza la wazee.
4. Mchungaji Msaidizi atafanya kazi anayopewa na Mchungaji kiongozi na hana mamlaka ya kuitisha kikao chochote bila idhini ya mchungaji kiongozi.
5. Mchungaji Msaidizi awe amemaliza masomo ya Shule ya biblia.

6. Kiongozi/Mchungaji wa PAG (T) haruhusiwi kugombea nafasi yeyote ya kisiasa na akifanya hivyo atakuwa amejiondoa katika nafasi ya uongozi/uchungaji.
7. Muda wa kipindi cha Makabidhiano kwenye ngazi ya Taifa, Jimbo na Wilaya ni mwezi moja.
8. Kutakuwa na Fomu iliyoandaliwa Halmashauri Kuu kwa ajili ya Makabidhiano kwa ngazi zote.
9. Fomu hiyo Makabidhiano itajazwa na anayekabidhi na kusainiwa na anayekabidhiwa, anayekabidhi na msimamizi wa Makabidhiano.
10. Baada ya uchaguzi mkuu, katika kipindi cha miaka minne. Wilaya itafanya mikutano miwili, Jimbo moja, Taifa moja wa uamsho kabla ya Mkutano Mkuu wa uchaguzi. Mwaka wa Uchaguzi mkuu hakutakuwa na mikutano kwa ngazi Taifa hadi wilaya. Idara zote kwenye ngazi ya Wilaya, Jimbo,Taifa zitafanya vivyo hivyo.
11. PAG (T) itatoa vyeti vifuatavyo:
    a) Cheti cha Msimikwa.
    b) Cheti cha Ubatizo.
    c) Cheti cha Kubariki watoto.
    d) Barua ya Safari.
    e) Cheti cha Uongozi.

f) Cheti cha Shukrani (Award Certificate of Appreciation).

g) Cheti cha Ndoa.

h) Cheti cha ushirika.

12. Halmashauri kuu ya PAG (T) itatoa Vitambulisho vifuatavyo:

a) Vitambulisho vya Wachungaji na wenzi wao.

b) Vitambulisho vya Viongozi.

c) Vitambulisho vya Watumishi waajiriwa.

13. Watoto wa Watumishi /Wachungaji watakuwa na mikutano yao ya pamoja katika ngazi ya Wilaya, Jimbo na Taifa, wakipata mafundisho ya kiroho.

14. Kila Kanisa litakuwa na mashemasi kutegemeana na ukubwa wa kanisa.

a ) Watateuliwa na Mchungaji.

b) Sifa zao zitakuwa sawa na (1Timotheo 3:8-13, Matendo ya Mitume 6:3-6).

c) Kazi za mashemasi.

i. Kusimamia ibada.

ii. Kuhesabu sadaka wakisimamiwa na Mhasibu.

iii. Kuelekeza wageni.

iv. Kuelekeza watu mahali pa kukaa.

v. Kuona mazingira ya kanisa yapo vizuri na salama.

vi. Kusimamia utulivu wa ibada.
vii. Watawajibika kwa Mchungaji.
viii. Watadumu kwa miaka miwili.
ix. Mchungaji kiongozi aweza kumwondoa Shemasi muda wowote akishirikiana na kamati ya kanisa.

15. Kanisa la PAG (T) linaruhusu wanawake kutumika katika huduma zote sawa na wito wao, wale wenye wito watawekwa wakfu kwa utumishi isipokuwa kwa wale wenye huduma ya uchungaji hawataruhusiwa kufanya mambo yafuatayo: Kufunga ndoa, Kushirikisha meza ya Bwana, Kubatiza, Kuweka watoto wakfu, waweza kuendesha ibada ya mazishi.
16. Kila uongozi katika ngazi zote kutakuwa na kitabu chenye Orodha ya Samani au mali walizonazo kila mwaka.
17. Wachungaji/Watumishi wote wa PAG (T) wanapaswa kujaza fomu ya "Makubaliano ya huduma kati ya Wachungaji na Kanisa".

18. PAG (T) inakubali kuwepo na Uhamisho kwa Wachu ngaji/Watumishi na hakuna sheria ya kuhamisha Wachungaji/Watumishi bila sababu. Sababu za Uhamisho kwa watumishi ni:

    a) Mchungaji mwenyewe kuomba kuhamishwa.

b) Ikiwa hali ya kiafya ni mbaya kutokana na hali ya hewa ya mahali alipo na uthibitisho wa cheti cha daktari utahitajika.

c) Kamati husika kuona haja ya kupeleka Mchungaji mwingine ili kuiponya kazi ya mahali pale.

d) Huduma yake kuhitajika mahali pengine.

e) Gharama ya Uhamisho zitalipwa na kamati amb ayo inamuhamisha Mchungaji.

f) Kamati yoyote isimhamishe Mchungaji kama haina gharama za uhamisho.

g) Mtumishi akifikia umri wa miaka 60 asihamishwe /kuondolewa katika kanisa analoongoza mpaka pawepo sababu maalumu isiyozuilika.

h) Mchungaji akihamishwa apelekwe kwenye kanisa lenye hadhi sawa au inayokaribiana na lile ambalo akilichunga.

i) Gharama ya uhamisho itatolewa na kamati husika kwa maelewano na Mchungaji anayehamishwa zitakuwa:

i. Nauli kwa Mchungaji, Mwenzi wake, Watoto na Mfanyakazi.
ii. Mizigo aliyonayo Mtumishi bila Mifugo.
iii. Gharama za kuhamisha watoto shuleni na kuwatafutia shule.
iv. Chakula cha njiani.

19. Watumishi/Wachungaji wa PAG (T) waweza kustaafu.
   a) Kanisa laweza kumsaidia kila mwezi kadiri iwezekanavyo.
   b) Aweza kukatiwa bima ya afya.
20. Kanisa la PAG linaruhusu kuvaa kola kwa Wachungaji wake, shati nyekundu ni kwa maaskofu na shati nyeusi au zambarau ni kwa ajili ya Wachungaji. Hata hivyo ni muhimu sana mchungaji avae kwa unadhifu kutegemeana na mazingira ya huduma yake.